**SHERIA YA KUWEKA MASHARTI YANAYOHUSIANA NA HAKI NA HUDUMA ZA USTAWI KWA WAZEE, NA KUANZISHA MPANGO WA PENSHENI JAMII, USIMAMIZI WAKE NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**


**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA PILI**
**MISINGI YA JUMLA, HAKI, STAHIKI NA WAJIBU**

4. Misingi ya jumla.
5. Haki za msingi za mzee.
6. Haki ya kuwakilishwa kisheria.
7. Haki ya kutambuliwa katika kupata huduma za kijamii.
8 Haki ya hadhi ya ubinaadamu.
9. Haki ya hifadhi na usalama wa mzee.
10. Haki ya afya.
11. Haki ya kupata habari.
12. Haki ya kuruhusiwa kuingia katika maeneo ya umma na binafsi.
13. Haki ya michezo, burudani, kupumzika na tamaduni.
14. Haki ya faragha.

15. Haki za kumiliki mali.

16. Msaada kwa wazee wanaohudumia watoto wenye mazingira magumu.

17. Wajibu wa mzee.

18. Wajibu wa familia.

19. Wajibu wa jamii.

## SEHEMU YA TATU
## WAZEE WANAOHITAJI MATUNZO NA HIFADHI

20. Mzee anayehitaji matunzo na hifadhi.

21. Wajibu wa kutoa taarifa.

22. Kosa dhidi ya mzee.

## SEHEMU YA NNE
## HUDUMA ZA MATUNZO NA MSAADA WA KIJAMII KWA WAZEE

23. Kuanzisha huduma za matunzo na msaada wa kijamii.

24. Haki za mzee katika huduma za matunzo na msaada wa kijamii.

25. Ufuatiliaji na tathmini ya huduma za matunzo na msaada wa kijamii.

## SEHEMU YA TANO
## USAJILI WA MAKAAZI YA WAZEE

26. Maombi kwa ajili ya usajili.

27. Kukataa kusajili.

28. Kusitisha au kufuta usajili.

29. Mapitio.

30. Jukumu la Serikali.

## SEHEMU YA SITA
## MPANGO WA PENCHENI JAMII

31. Kuanzishwa kwa Mpango wa Pencheni Jamii.

32. Kiwango.

33. Maombi na sifa za kuingizwa katika Mpango wa Pencheni Jamii.

34. Kusitishwa au kuondolewa.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI MENGINEYO

35. Uanzishwaji wa jumuiya au taasisi za wazee.

36. Adhabu ya jumla.

37. Kanuni.

**SHERIA NAM. 2 YA 2020**

**NIMESAINI**

**{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

6 Machi, **2020**

# SHERIA YA KUWEKA MASHARTI YANAYOHUSIANA NA HAKI NA HUDUMA ZA USTAWI KWA WAZEE, NA KUANZISHA MPANGO WA PENSHENI JAMII, USIMAMIZI WAKE NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Masuala ya Wazee, 2020 na itaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Rais na tarehe ambayo itatangazwa na Waziri katika Gazeti la Serikali.

Matumizi.

**2.** Sheria hii itatumika kwa wazee, taasisi na makaazi yanayotoa huduma kwa wazee ndani ya Zanzibar.

Ufafanuzi.

**3.** Katika Sheria hii, isipokuwa maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Udhalilishaji" maana yake ni aina mbali mbali za vitendo au tabia mbaya dhidi ya wazee kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 22(2);

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Masuala ya Wazee, 2020;

"Vifaa vya usaidizi" maana yake ni vifaa na nyenzo zinazotolewa kwa mzee kumwezesha kufanya shughuli zake za kila siku;

"Huduma za msingi" zinajumuisha utoaji wa chakula, huduma za afya, makaazi, usafi wa mwili na maji;

"Matunzo" maana yake ni usaidizi wa kimwili, kiakili, kijamii au msaada wa kifaa kwa mzee, na inajumuisha huduma zinazolenga katika kuimarisha maisha na ustawi wa jumla wa mzee;

"Mtoa matunzo" maana yake ni mtu anayetoa matunzo kwa mzee;

"Huduma za matunzo na msaada wa kijamii" maana yake ni mpango wowote ulioanishwa katika Sehemu ya Nne ya Sheria hii;

"Mzee" maana yake ni mtu yeyote mwenye umri wa miaka 70 au zaidi;

"Mzee anayehitaji matunzo na hifadhi" maana yake ni mtu kama alivyoainishwa katika Sehemu ya Tatu ya Sheria hii;

"Familia" maana yake ni kundi la watu wenye uhusiano wa damu, ndoa au kuasili na mzee;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Mtoa huduma za afya" maana yake ni mtoa huduma za afya kama ilivyotafsiriwa katika sheria za Zanzibar;

"Huduma za matunzo ya nyumbani" maana yake ni matunzo au huduma zinazotolewa na mtoa matunzo katika eneo analoishi mzee asiyejiweza ili kuhakikisha anapata huduma inayoridhisha mpaka kufikia mwisho wa maisha yake, isipokuwa wazee waliokuwepo katika makaazi;

"Makaazi" maana yake ni makaazi ya wazee yanayotoa huduma kwa wazee;

"Serikali za Mitaa" maana yake ni serikali za mitaa kama zilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na masuala ya wazee;

"Wizara" maana yake ni Wizara inayohusika na masuala ya wazee;

"Pencheni" maana yake ni malipo yalioainishwa katika Sehemu ya Sita ya Sheria hii;

"Mpokeaji pencheni" maana yake ni mtu anayestahiki kupokea pencheni jamii;

"Urekebishaji" maana yake ni utaratibu unaomuwezesha mzee kufikia na kuimarisha hali yake kimwili, kihisia, ufahamu, kiakili au kijamii;

"Mpango" maana yake ni Mpango wa Pencheni Jamii Zanzibar;

"Watoa huduma" maana yake ni makaazi au mtu ambae anatoa huduma zilizowekwa kukidhi mahitaji ya mzee;

"Huduma" maana yake ni shughuli yoyote au mpango uliowekwa kukidhi mahitaji ya mzee;

"Hifadhi" maana yake ni jengo au maeneo yaliyowekwa au yanayotumika kwa ajili ya kupokea, kuhifadhi na kutoa matunzo ya muda kwa mzee anayehitaji matunzo na hifadhi;

"Msaada wa kijamii" maana yake ni maslahi katika namna ya kitu au uhaulishaji unaofanywa na Serikali au taasisi ya kiraia au watu binafsi kwa kaya kufikia mahitaji ya msingi ya wazee;

## SEHEMU YA PILI
## MISINGI YA JUMLA, HAKI, STAHIKI NA WAJIBU

Misingi ya jumla.

**4.**-(1) Mwenendo wa kesi zote, hatua au maamuzi katika jambo linalohusiana na mzee:

(a) yataheshimu, yatahifadhi, yataimarisha na yatatambua haki za wazee, maslahi bora ya mzee na haki na misingi iliyowekwa katika Sheria hii, kwa kuzingatia mipaka ya kisheria;

(b) yataheshimu hadhi ya wazee inayostahiki;

(c) yatamtendea mzee kwa haki na usawa; na

(d) yatamlinda mzee dhidi ya aina yoyote ya ubaguzi na udhalilishaji.

Haki za msingi za mzee.

**5.** Mbali na haki nyengine zilizotajwa katika Sheria hii, Mzee katika jamii atakuwa na haki za msingi zifuatazo:

(a) kushiriki katika masuala ya kijamii katika nafasi yoyote inayomstahiki kwa maslahi na uwezo wake;

(b) kuanzisha na kushiriki katika jumuiya zinazohusika na wazee;

(c) kushiriki katika shughuli zitakazomuwezesha kupata kipato chake;

(d) kuishi katika mazingira yanayoendana na mabadiliko ya hali yake;

(e) kupata fursa ambazo zitakuza kiwango chake cha ustawi kijamii, kimwili, kiakili na kihisia;

(f) kuendeleza maendeleo yake binafsi;

(g) kusimamia mali yake;

(h) kuishi kwa hadhi na kuwa huru dhidi ya udhalilishaji;

(i) kupokea matunzo yanayofaa na msaada kutoka katika familia yake, Serikali au mtu mwengine yeyote;

(j) kupata huduma zinazohusiana na shughuli za hifadhi ya jamii; na

(k) kusajiliwa katika daftari la wazee.

Haki ya kuwakilishwa kisheria.

**6.**-(1) Mzee ana haki ya kuwakilishwa kisheria na haki ya kushiriki katika hatua zote na kupata msaada muhimu kwa ajili ya kuwakilishwa kisheria.

(2) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mzee ana haki ya kupatiwa ushauri wa kisheria katika masuala ya kijamii.

Haki ya kutambuliwa katika kupata huduma za kijamii.

**7.** Mzee ana haki ya kupatiwa kitambulisho ambacho kitamuwezesha kupata huduma muhimu za jamii na hati nyengine yoyote ya utambulisho.

Haki ya hadhi ya ubinaadamu.

**8.** Mzee ana haki ya kuishi kwa hadhi, usalama, kuwa huru dhidi ya unyonyaji na udhalilishaji wa kimwili au kiakili.

Haki ya hifadhi na usalama wa mzee.

**9.** Mzee ana haki ya hifadhi inayofaa na maalumu na usalama katika hali za hatari, ikijumuisha hali ya kivita, maafa na matukio ya majanga ya kiasili.

Haki ya afya.

**10.**-(1) Mzee ana haki ya kupata huduma za afya bila ya malipo na matibabu maalum katika hospitali na kituo chochote cha afya cha umma na atapewa kipaumbele kupatiwa huduma hizo.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Serikali inaweza kwa kuzingatia uwezo wa kifedha kuingia makubaliano kwa madhumuni ya kuwawezesha wazee kupata matibabu katika hospitali binafsi.

Haki ya kupata habari.

**11.** Mzee ana haki ya kupata habari ambayo ni muhimu kwa maslahi na ustawi wake.

Haki ya kuruhusiwa kuingia katika maeneo ya umma na binafsi.

**12.**-(1) Mzee ana haki ya:

(a) kuruhusiwa kuingia katika maeneo yoyote ambayo wananchi kikawaida wanaruhusiwa; au

(b) kupatiwa huduma na mahitaji ambayo wananchi wanastahiki.

(2) Mmiliki wa maeneo binafsi ambayo yanatoa huduma za kijamii hatoizuia haki ya mzee kuingia katika maeneo yake.

Haki ya michezo, burudani, kupumzika na tamaduni.

**13.**-(1) Mzee ana haki ya kushiriki katika shughuli za michezo, burudani, mapumziko na tamaduni zikiwemo matukio ya michezo ya Kitaifa na Kimataifa.

(2) Mzee anastahiki kutumia bila ya malipo huduma za michezo na burudani zinazomilikiwa au kuendeshwa na Serikali wakati wa sherehe za shughuli za kijamii, michezo na burudani.

(3) Kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, hakitatumika pale ambapo huduma hizo zitatolewa na mtu binafsi.

Haki ya faragha.

**14.**-(1) Mzee hatakiwi kuingiliwa bila ya sababu ya msingi katika masuala yake ya faragha, familia, nyumbani au mawasiliano ya barua au aina nyengine za mawasiliano.

(2) Makaazi ya umma au binafsi yatatunza taarifa za siri za binafsi, za afya na za urekebishaji wa mzee.

Haki za kumiliki mali.

**15.**-(1) Mzee ana haki ya kumiliki na kutoa mali yake kwa namna ambayo anaona inafaa kwa mujibu wa uwezo wake.

(2) Mzee ana haki ya kuelimishwa kuhusiana na umuhimu wa kuweka wasia na uwakala kwa ajili ya kulinda mali yake.

Msaada kwa wazee wanaohudumia watoto wenye mazingira magumu.

**16.** Waziri ataweka utaratibu wa kuwasaidia wazee ambao wanawahudumia watoto wenye mazingira magumu.

Wajibu wa mzee.

**17.**-(1) Kila mzee ana wajibu kwa familia yake, jamii, Serikali na taasisi za kimataifa.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mzee:

(a) atatoa mafunzo na kuwapatia elimu na uzoefu watoto na vijana;

(b) atawezesha majadiliano na mshikamano ndani ya familia yake na jamii; na

(c) atachukuwa jukumu la upatanishi na usuluhishi wa migogoro.

(3) Mzee hatotumia vibaya haki au fursa zilizotolewa chini ya Sheria hii.

Wajibu wa familia.

**18.** Katika kumtunza mzee, familia ambayo mzee anaishi itakuwa na wajibu wa:

(a) kutoa upendo, huruma, chakula, hifadhi na kumpatia mahala pa kuishi;

(b) kusaidia jitihada za Serikali na serikali za mitaa katika kutoa gharama za matibabu kwa ajili ya mzee aliyepata maradhi na kumpatia huduma za uangalizi;

(c) kumwezesha kuishi na mwenza wake isipokuwa kama kuna mazingira yanayolazimisha kutenganishwa;

(d) kuendeleza umiliki wa mali zake zikiwemo nyumba, shamba au mapato mengine yoyote yanayotokana na mali anazozimiliki; na

(e) kutoa msaada wowote unaofaa kila unapohitajika.

Wajibu wa jamii.

**19.** Jamii itakuwa na wajibu wa kulinda maslahi bora ya wazee katika jamii.

## SEHEMU YA TATU
## WAZEE WANAOHITAJI MATUNZO NA HIFADHI

Mzee anayehitaji matunzo na hifadhi.

**20.** Mzee anayehitaji matunzo na hifadhi ni ambaye:

(a) aliyeondolewa kutoka katika makaazi yake bila ya ridhaa yake au kinyume na sheria amepokonywa mali yake anayomiliki kihalali;

(b) aliyetelekezwa au aliyetupwa bila ya msaada wowote;

(c) anaishi au anazurura mitaani au anaomba omba kwa ajili ya kuishi;

(d) anatumia au ameathirika na dawa za kulevya na bila ya kupata msaada wowote au huduma ya kuacha matumizi ya dawa za kulevya;

(e) anaishi katika mazingira ambayo yanapelekea au yanasababisha kutekwa au kudhalilishwa ikiwemo udhalilishaji wa kingono au kiuchumi;

(f) anaishi au yupo katika mazingira yanayoweza kusababisha madhara ya kimwili au kiakili au yupo katika hali ya kutelekezwa kimwili, kiakili au kijamii; au

(g) yupo katika mazingira mengine yoyote ambayo Wizara inaona kuwa mzee anastahiki.

Wajibu wa kutoa taarifa.

**21.**-(1) Mtu ambaye ana sababu ya msingi ya kuamini kwamba mzee anahitaji matunzo na hifadhi atatoa taarifa hiyo ama kwa:

(a) Sheha;

(b) Kituo cha Polisi;

(c) Afisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya;

(d) Jumuiya au taasisi ya wazee inayotambulika; au

(e) Wizara.

(2) Kwa kuzingatia masharti yaliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (1)(a) na (b) cha kifungu hiki, taarifa iliyotolewa italazimika kuwasilishwa kwa Afisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya au wizara husika.

Kosa dhidi ya mzee.

**22.**-(1) Mtu anayemdhalilisha au anayesababisha kudhalilishwa mzee atakuwa ni mkosa na akitiwa hatiani atahukumiwa kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi na nne au faini isiyopungua Shilingi Milioni Mbili au adhabu zote mbili.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, "udhalilishaji" unajumuisha wa kimwili, kingono na kiakili, na:

(a) "udhalilishaji wa kimwili" maana yake ni kitendo chochote au vitisho vya ukatili wa kimwili dhidi ya mzee;

(b) "udhalilishaji wa kingono" maana yake ni kitendo chochote kinachovunja heshima ya kijinsia ya mzee na kosa jengine lolote chini ya Sheria ya Adhabu;

(c) "udhalilishaji wa kiakili" maana yake ni kitendo cha kushusha hadhi au kumtia aibu mzee, ikijumuisha:

(i) matusi yanayojirejea, dharau au kuita jina baya;

(ii) vitisho vinavyojirejea au kumsingizia uongo ambao unaweza kusababisha maumivu ya kihisia; na

(iii) kuingia kwa nguvu kunakojirejea kwenye faragha, uhuru, heshima au usalama wa mzee.

## SEHEMU YA NNE
## HUDUMA ZA MATUNZO NA MSAADA WA KIJAMII KWA WAZEE

Kuanzisha huduma za matunzo na msaada wa kijamii.

**23.**-(1) Mamlaka ya Serikali ya Mtaa inaweza kuanzisha huduma za matunzo na msaada wa kijamii kwa lengo la kuwahudumia wazee wanaoishi katika eneo lake.

(2) Waziri anaweza kutoa muongozo juu ya kuanzishwa kwa huduma za matunzo na msaada wa kijamii.

(3) Msaada wa kijamii ulioanishwa katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki unaweza kujumuisha:

(a) msaada wa kisheria;

(b) msaada wa kisaikolojia;

(c) huduma za afya;

(d) uangalizi; na

(e) msaada mwengine wowote kutegemea na mazingira ya mzee.

Haki za mzee katika huduma za matunzo na msaada wa kijamii.

**24.** Mzee anayepata huduma za matunzo na msaada wa kijamii, pamoja na haki zilizoainishwa katika Sehemu ya Pili ya Sheria hii, ana haki ya:

(a) kuishi katika familia au makaazi kwa kadiri iwezekanavyo;

(b) kupata fursa za kumuendeleza kufikia uwezo wake kamili; na

(c) kufaidika na matunzo na hifadhi kutoka katika familia na jamii kwa mujibu wa mila, utamaduni na desturi.

Ufuatiliaji na tathmini ya huduma za matunzo na msaada wa kijamii.

**25.**-(1) Wizara itafuatilia na kutathmini huduma za matunzo na msaada wa kijamiii.

(2) Utaratibu wa ufuatiliaji na tathmini ya huduma hizo utaelezwa katika Kanuni.

## SEHEMU YA TANO
## USAJILI WA MAKAAZI YA WAZEE

Maombi kwa ajili ya usajili.

**26.**-(1) Makaazi ya wazee hayatatoa huduma bila ya kupata usajili rasmi.

(2) Taratibu za usajili zitaelezwa katika Kanuni zitakazoandaliwa na Waziri.

Kukataa kusajili.

**27.** Wizara inaweza, ikiwa imeridhika kwamba muombaji ameshindwa kukidhi masharti ya usajili yaliyoelezwa katika Kanuni, kukataa kumsajili muombaji huyo, na itamjulisha muhusika kwa maandishi sababu za kukataa huko.

Kusitisha au kufuta usajili.

**28.**-(1) Endapo makaazi ya wazee yaliyoidhinishwa yameshindwa kufikia vigezo vinavyohitajika, Wizara inaweza kusitisha au kufuta usajili.

(2) Kabla ya kusitisha au kufuta usajili, Wizara:

(a) itamjuilisha muombaji kwa maandishi nia ya kusitisha au kufuta usajili; na

(b) itampa muombaji fursa ya kusikilizwa au kuwakilishwa.

(3) Wizara inaweza, kwa taarifa ya maandishi, kumtaka muombaji kurekebisha makosa katika uendeshaji wa makaazi.

(4) Endapo muombaji anashindwa kukidhi masharti ya taarifa iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, wizara inaweza kuendelea na kusitisha au kufuta usajili huo.

Mapitio.

**29.** Mtu ambaye hakuridhika na maamuzi ya Wizara ya kukataa kumpatia muombaji usajili, kusitisha usajili au kufuta usajili chini ya Sehemu hii, anaweza kuomba mapitio kwa Waziri ndani ya siku thelathini kutoka tarehe ya kukataa au kusitisha au kufuta.

Jukumu la Serikali.

**30.**-(1) Wizara itafuatilia na kusimamia kuhakikisha kwamba makaazi yote ya wazee yanakuwa katika hali nzuri na kuendeshwa ipasavyo.

(2) Waziri ataanzisha utekelezaji wa sera na programu zinazohusiana na wazee.

## SEHEMU YA SITA
## MPANGO WA PENCHENI JAMII

Kuanzishwa kwa Mpango wa Pencheni Jamii.

**31.** Kunaanzishwa Mpango wa Pencheni Jamii ambao utaratibiwa na Wizara.

Kiwango.

**32.**-(1) Kutakuwa na kiwango kitakachotolewa kwa kila mzee ambaye anastahiki kupokea pencheni kutoka katika Mpango wa Pencheni Jamii.

(2) Kiwango kilichoelezwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kitalipwa kila mwezi.

(3) Waziri, baada ya idhini ya Baraza la Mapinduzi, atatangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali kiwango cha kulipwa wazee.

Maombi na sifa za kuingizwa katika Mpango wa Pencheni Jamii.

**33.**-(1) Mzee ataomba katika Wizara kupitia Sheha wake na Mkuu wa Wilaya kuingizwa katika Mpango wa Pencheni Jamii.

(2) Mzee hatokuwa na sifa ya kuomba kuingizwa katika Mpango wa Pencheni Jamii isipokuwa mzee huyo:

(a) ana umri wa miaka sabini au zaidi;

(b) ni Mzanzibari; na

(c) amekuwa mkaazi wa Zanzibar kwa zaidi ya miaka kumi mfululizo.

(3) Maombi yanayofanywa chini ya kifungu kidogo cha(1) cha kifungu hiki yataambatana na mambo yafuatayo:

(a) picha mbili ndogo za karibuni;

(b) cheti cha kuzaliwa au hati ya kiapo cha kuzaliwa; na

(c) Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

(4) Umri uliotajwa katika kifungu kidogo cha (2)(a) unaweza kupunguzwa au kuongezwa na Waziri kwa kushauriana na Baraza la Mapinduzi.

Kusitishwa au kuondolewa.

**34.**-(1) Mpokeaji pencheni atasita au kuondolewa kupokea pencheni ya mwezi ikitokea moja kati ya mambo yafuatayo:

(a) kifo;

(b) hadaa; au

(c) udanganyifu.

(2) Utaratibu wa kutoa taarifa kuhusiana na matukio yaliyoainishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utaelezwa katika Kanuni.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI MENGINEYO

Uanzishwaji wa jumuiya au taasisi za wazee.

**35.**-(1) Wizara inaweza kushauri uanzishaji wa jumuiya au taasisi huru za wazee.

(2) Katika kuanzisha jumuiya au taasisi, wazee watazingatia mambo yafuatayo:

(a) jumuiya au taasisi iwafanye wazee kuwa pamoja katika kulinda maslahi yao;

(b) kuratibu mashirikiano kati ya wazee na Serikali, sekta binafsi, jumuiya za kiraia na taasisi nyengine zenye maslahi yanayolingana;

(c) kuhamasisha na kushauri Serikali katika ngazi ya taifa na serikali ya mtaa katika mambo mbali mbali yenye maslahi ya jamii; na

(d) kuelekeza na kuongoza watoto na vijana katika jamii.

Adhabu ya jumla.

**36.** Mtu anayekwenda kinyume na kifungu chochote cha Sheria hii, isipokuwa kifungu cha 17(1) ambacho haikutajwa adhabu yake maalum, atatozwa faini isiyozidi Shilingi Milioni Moja au kifungo cha kipindi kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote mbili.

Kanuni.

**37.** Waziri anaweza kutunga Kanuni katika jambo lolote ambalo ni muhimu kwa utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 6 Februari, 2020.

..................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***